OneHope
God's Word. Every Child.



# UTAMADUNI
## WA VIJANA DUNIANI
*Uelewa Wa Kizazi Cha Kidijitali*

# *Yaliyomo*

3 UTANGULIZI

5 MITAZAMO YA KIDINI NA TABIA
16 UZOEFU NA MAHANGAIKO BINAFSI
25 MUUNGANIKO KIDIJITALI NA MADHARA YAKE
33 UTAMBULISHO NA MAHUSIANO
44 USHAWISHI NA SAUTI ZA MWONGOZO

53 BARUA YA ROB HOSKINS
54 KUHUSU ONEHOPE
54 NJIA ZA KUFUNDISHIA
55 UKUSANYAJI WA TAARIFA
56 UFAFANUZI WA MANENO

# UTANGULIZI

Kizazi cha sasa cha vijana duniani kilizaliwa kati ya 1995-2012. Kizazi hiki kina vijana takribani bilioni 2 ambao ni 25% ya idadi ya watu duniani.[1] Vijana hawa wana mitazamo ya kipekee na tofauti juu ya uzoefu wa kimaisha na ulimwengu wanaokulia.

Utafiti huu umeweka wazi tabia, mahangaiko, imani na ushawishi wa kizazi hiki duniani. Takwimu hizi pia zinaweka bayana mawazo yao juu ya Mungu, Yesu, Biblia, na Kanisa la Kikristo. Tunaamini kuwa utafiti huu ni mtambuka kwa aina yake kwa namna ulivyotazama kwa undani imani ya vijana Ulimwenguni. Mamia ya takwimu tulizokusanya kutoka kwa maelfu ya vijana duniani zinajenga taswira ya kizazi hiki na kuibua ugunduzi wa kushangaza pamoja na visa visivyomulikwa.

Nchi 20

Lugha 14

Vijana Waliunganika Kidijitali 8,394

Umri 13-19

Mambo 70 Yalifanyiwa Utafiti



**Afrika:** Kenya, Nigeria, Afrika Kusini (Vijana 1,275 walifanyiwa utafiti)

**Asia:** China, India, Indonesia, Japani, Vietnam (Vijana 2,100 walifanyiwa utafiti)

**Ulaya** Misri, Uholanzi, Ureno, Romania, Urusi, Hispania, Uingereza (Vijana 2,936 walifanyiwa utafiti)

**Amerika ya Kusini:** Argentina, Brazili, Colombia, Mexico (Vijana 1,673 walifanyiwa utafiti)

**Amerika ya Kaskazini:** Marekani (Vijana 410 walifanyiwa utafiti)

---

*1 United Nations Population Division https://esa.un.org/unpd/wpp/DataQuery/*

# KUHUSU VIJANA

**WAKIUME** *51%*
**WAKIKE** *49%*

**UMRI**

| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| *5%* | *4%* | *6%* | *13%* | *15%* | *27%* | *30%* |

## DINI ZINGINE **23%**

- *Waislamu 12%*
- *Wabudha 5%*
- *Wahindu 4%*



## WAKRISTO **43%**

## WASIO NA DINI **34%**

- *Wasioamini Kuna Mungu 15%*
- *Hakuna 13%*
- *Wasioamini Mungu Anatambulika 5%*

Dodoso ziligawanywa mtandaoni kwa makundi ya vijana wenye umri 13-19 ambao wanakuwa na fursa ya intaneti mara kwa mara. Tambua kuwa matokeo haya sio maoni au msimamo wa vijana wote, isipokuwa wale wenye muunganiko wa kidijitali. Takwimu zilikusanywa kati ya Februari 24 – Machi 27, 2020—kabla ya madhara ya janga la korona hayajasambaa kote. Matokeo yake, utafiti huu unadhihirisha imani na tabia za vijana kabla ya marufuku ya kutoka nje haijaanza kutekelezwa.

### *Kutoka Kwenye Timu ya Utafiti*

Tunatumaini kuwa sio tu utajifunza kitu kipya kutokana na utafiti huu, bali pia moyo na akili yako vitasukumwa kufanya jambo kwa niaba ya kizazi hiki—ambacho kama kizazi kingine chochote—kinahitaji tumaini la Injili maishani mwao. Kila takwimu kwenye utafiti huu inawakilisha vijana wengi wakiwa na matumaini yao, hofu zao, na mahangaiko yao. Kila mmoja wa hao vijana ana jina, kisa, na hatima ya milele. OneHope imejitoa kugusa hatima hizo kwa kumuunganisha kila kijana na Yesu kupitia Neno Lake.

# MITAZAMO NA TABIA ZA KIDINI

# Tulichogundua

## VIJANA ULIMWENGUNI...



**Zaidi ya nusu** (52%) ya vijana duniani wanasema **hawasomi Maandiko ya kidini wenyewe.**

Vijana wasiokwenda kanisani wanasema **wako tayari kuhudhuria kama wakialikwa** na kwamba Wakristo wanaowafahamu ni **wakarimu na wanaojali.**

Zaidi ya nusu (52%) ya vijana wanaamini **kuwa dini zote hufundisha ukweli halisi.** Kwa kusema hivi, inaonekana Wakristo **wapo sawa tu** na wasioamini.

**Wawili kati ya vijana watatu** ulimwenguni wanasema Imani zao au safari ya kiroho ni sehemu **muhimu ya utambulisho wao.**

Vijana wa Kiislamu katika utafiti wetu ndio **wenye nidhamu zaidi** kuliko dini nyingine yoyote kuhusiana na **kuhudhuria ibada, kusoma maandiko, na kuomba.**



## VIJANA WA KIKRISTO

**43%** ya vijana waliotafitiwa **wanajitambulisha kuwa Wakristo.**





Ni **7%** tu wanaodhihirisha imani na tabia za **Wakristo Imara.**

*(Ona ufafanuzi ukurasa wa 8)*

**40%** ya vijana wanaojitambua kama Wakristo wanasema **hawasomi Biblia.**

Vijana wenye Imani halisi ya Kikristo, mara kwa mara husoma Biblia, na wenye tabia za maombi **wana kiwango kidogo cha mahangaiko binafsi.**


# Mitazamo Na Tabia Za Kidini

Utafiti huu kwa kipekee ulizama katika kupima namna ambavyo Imani na dini vinaathiri maisha ya vijana wengi leo.

Je, Safari ya Imani ni muhimu kwao kwa kiwango gani? Wanaweka imani zao kwenye matendo? Utafiti huu unachokonoa mitazamo na tabia za vijana leo na matokeo yake kwenye maeneo mengine ya maisha yao.

## UTAMBULISHO WA KIDINI DUNIANI

Duniani, takribani vijana 2 kati ya 5 wanajitambua kama Wakristo, 1 kati ya 4 kama dini zingine, na 1 kati ya 3 kama wasio na dini, wasioamini kuna Mungu au wanaoamini Mungu hawezi kutambulika. Kwenye dini zote tulizotafiti, Afrika ilikuwa na Wakristo wengi na Asia wachache.



# *Walio Imara Wachache*

Baadhi ya matokeo ya kushangaza katika utafiti huu yalijitokeza tulipojikita kwa vijana wa Kikristo waliomaanisha kwenye Imani na desturi za Kikristo. Tuligundua kuwa kujiita Mkristo kunatofautiana kikubwa kutoka mtu hadi mtu, mazingira waliopo, na utamaduni wao. Kwa malengo ya utafiti huu, OneHope iliandaa ufafanuzi wa imani na tabia zinazoashiria kuwa mhusika ni Mkristo Imara.

## TABIA 6 YA VIJANA WAKRISTO IMARA

- Wanaamini Mungu yupo na wanaweza kujenga mahusiano binafsi na Yeye
- Wanaomba walau mara moja kwa wiki
- Wanasoma Maandiko wenyewe walau mara moja kwa wiki



- Wanaamini Yesu ni Mwana wa Mungu
- Wanaamini msamaha wa dhambi unapatikana tu kupitia imani kwa Yesu Kristo
- Wanaamini kuwa Biblia ni Neno la Mungu


** Fahamu kuwa vijana hao hujitambua kama Wakristo, lakini sio kama Mashahidi wa Yehova au Mormon. Wakristo Imara wanaweza kuwa Wakatoliki, Wasabato, Orthodox, au mengi ya madhehebu mengine.*

Duniani, takribani kijana 1 kati ya 14 wanaendana na huu ufafanuzi wa Wakristo Imara. Wakati 43% ya sampuli yetu wanatambua Ukristo kama dini, ni 7% tu wanaodhihirisha Imani na tabia zinazoashiria kuwa wana mwenendo wa Wakristo Imara. Vijana wakubwa wanaonekana kumaanisha zaidi kwenye Ukristo kuliko vijana wachanga. Ni 5% ya vijana kati ya umri wa miaka 13-15 ni Wakristo Imara; 6% kati ya umri 16-17; na 8% ya umri wa miaka 18-19.

## WAKRISTO IMARA KULINGANA NA UMRI

| 5% | 6% | 8% |
|---|---|---|
| 13-15 | 16-17 | 18-19 |

## WAKRISTO IMARA DUNIANI





**Wachache kuliko kijana 1 kati ya Vijana 14 dunia nzima wamemaanisha katika mambo ya msingi yanayohusu imani na tabia za Ukristo.**

***Wakristo wa Kawaida*** *ni vijana wanaojitambulisha kama Wakristo lakini hawaashirii tabia moja au zaidi kati ya imani au tabia za msingi za Mkristo Imara kama ilivyofafanuliwa ukurasa wa 8.*

## TABIA ZA KIDINI

Vijana Imara wa Kikristo hudhihirisha tabia na ushawishi tofauti wa kidini kuliko vijana wengine wa Kikristo—wanaojulikana kama Wakristo wa Kawaida katika utafiti huu. Wakristo Imara wana uwezekano mara tatu zaidi kuhudhuria kanisani walau mara moja kwa wiki kulinganisha na vijana ambao ni Wakristo wa Kawaida. Wanaamini kuwa wanawajibika kushirikisha imani yao kwa wengine, na wanauweka ushawishi huo kwenye matendo kwa kueneza Injili. Wakristo Imara wanaweza mara mbili zaidi kujihusisha na mazungumzo ya kiroho na wasioamini kuliko Wakristo wa Kawaida.




# Manufaa Ya Kumaanisha

Kiuhalisia, ni mabadiliko gani tunayoona kwenye Maisha ya Mkristo Imara? Takwimu zinaonesha kuwa Mkristo Imara ana manufaa chanya ambayo yako wazi.

## MAHANGAIKO BINAFSI

*Kwa miezi mitatu iliyopita, nimepitia:*





Ndani ya miezi mitatu iliyopita vijana Imara wa Kikristo walionesha uwezekano mdogo kuliko vijana wengine, kuwa na msongo, mawazo ya kujiua, au kujaribu kujiua. Wana uwezekano mdogo wa kuripoti kuwa wamechanganyikiwa juu ya utambulisho wao wa kijinsia au kwa hivi karibuni wamekuwa na mvuto wa mapenzi ya jinsia moja.

Wakristo Imara wana kiwango kidogo cha tabia hatarishi na hali ya kusikitisha ya afya ya akili kwa karibia kila jambo tulilopima, wakati Wakristo wa Kawaida walionekana kukaribia wastani wa vijana wote waliotafitiwa.

# Tabia za Vijana wa Kidini

Tulipima tabia za kidini za vijana kama kukusanyika na jumuiya zao za imani, kusoma Maandiko, na kuomba. Hapa kuna yale ambayo vijana wa Kiislamu,[1] Kikristo, na dini zingine[2] wanafanya kwenye maeneo haya.




---


*1 Idadi kubwa ya sampuli za jamii za Kiislamu zilichukuliwa kutoka Indonesia na Misri, na idadi ndogo kutoka Nigeria, India, na Kenya.*
*2 Angalia ukurasa 7 kwa kiwango cha mtawanyiko duniani kwa kila dini.*

## KUJIHUSISHA NA MAANDIKO




**52% ya vijana wanasema hawajawahi kusoma maandiko ya kidini wenyewe.**

## MAHUDHURIO KANISANI





Kati ya vijana wote tuliotafiti, Waislamu walikuwa wa kidini zaidi. Tisa kati ya vijana kumi wa Kiislamu wanasema imani yao ni sehemu muhimu katika utambulisho wao— kiwango cha juu kuliko vijana wa dini zingine. Vijana wa Kiislamu wanaonesha nidhamu zaidi kuhusiana na tabia zao za kidini. Asilimia sitini na moja ya vijana wa Kiislamu wanasema wanakwenda msikitini kila siku au kila wiki, wakati ni 36% ya Vijana wa Kikristo wanaosema wanakwenda kanisani kwa ibada kila mara. Zaidi ya kijana 1 kati ya 5 wa Kikristo wanasema hawajawahi kwenda kanisani.

Katika utafiti wetu vijana wa Kiislamu walionekana kuwa na nidhamu zaidi katika kusoma maandiko yao ya kidini na kuomba. Waislamu ni mara tatu zaidi kujihusisha na Quran kila siku (36%) kuliko vijana wa Kikristo ambao husoma Biblia kila siku (11%). Wawili kati ya vijana watano wa Kikristo hawajawahi kusoma Biblia wenyewe.




Kulinganisha mara ambazo wanasoma Maandiko, vijana wanaweza kusema kuwa wana tabia za kuomba. Bila kujali dini, 42% ya vijana wanasema huomba kila wiki au kila siku. Waislamu wana nidhamu zaidi, 72% wanasema wanaomba kila siku kulinganisha na 41% ya Vijana wa Kikristo na 33% ya vijana wa dini zingine.


# Kuwa Kiroho kama Utambulisho



**41%** ya vijana ambao tayari hawaendi kanisani wanasema wataenda kama wakialikwa.

**34%** wanasema hawana uhakika.

SIMJUI MKRISTO YEYOTE





Vijana dunia nzima wako wazi juu ya dhana ya kuwa kiroho, bila kujali dini zao. Wawili kati ya vijana watatu duniani husema imani zao au safari yao ya kiroho ni sehemu muhimu ya utambulisho wao. Takribani nusu (44%) ya vijana wasio na dini husema hili.

Vijana wanasema pia kuwa wanaweza kukubali kukaribishwa kanisani. Asilimia arobaini na moja ya vijana wasiokwenda kanisani wanasema watakwenda kama wataalikwa, na 34% ya wengine wanasema hawana uhakika. Ni 1 kati ya 4 anayesema kuwa hatakwenda. Hii inaashiria kuwa vijana leo ni watafutaji walio tayari kupata uzoefu wa kiroho popote wanapoweza kuupata.

Takwimu zinaweka wazi kuwa vijana wana mtazamo chanya juu ya watu wenye imani kwenye maisha yao. Asilimia sabini na moja ya vijana wasio wa Kristo wanasema Wakristo wengi wanaowafahamu ni wakarimu na wanajali. Hata hivyo, kwenye baadhi ya nchi za Asia, wanasema hawajui Mkristo hata mmoja.

## WAKO TAYARI KWENDA KANISANI



# *Wakati Kila Kitu Ni Kweli*

Vijana wengi leo hawako tayari kusema kuwa ukweli unapatikana kwenye dini moja tu. Zaidi ya nusu (52%) ya vijana duniani huamini kuwa dini zote hufundisha kweli halisi. Kati ya vijana wa Kikristo, kiwango cha kukubali ni 53%. Vijana wa baadhi ya dini, kama Uislamu, Ubudha, na Uhindu wana uwezekano wa kukubaliana na hili zaidi.

Labda haya ni matokeo ya hali ya utayari wa kiroho wa kizazi hiki, kwani mtazamo huu unaonekana kushikiliwa na vijana wengi kwenye dini na maeneo mengi. Hakika, kama imani ni sehemu muhimu ya utambulisho wao, vijana wana uwezekano zaidi— sio chini¬— kuwa na msimamo huu (67%). Hili linatupeleka kwenye kitendawili cha kizazi cha leo. Vijana wengi wanakubali kuwa safari ya kiroho ni sehemu muhimu ya utambulisho wao pasipo kufahamu kwa hakika ni wapi ukweli unapatikana. Hata vijana wa Kikristo wanaonekana kushawishika na fikra hizi. Idadi ndogo (30%) hawakubaliani na maelezo kuwa msamaha wa dhambi unawezekana tu kupitia imani ndani ya Yesu Kristo.


**52% ya vijana duniani huamini kuwa dini zote hufundisha kweli halisi.**

**46% ya vijana wanasema hawajawahi kushirikisha mambo ya dini wala kiroho kwa wengine ambao hawashiriki imani yao.**

Imani za kiroho kwa sehemu kubwa ni suala binafsi na sio jumuiya. Karibia nusu (46%) ya vijana wanasema hawajawahi kushirikisha mambo ya dini wala kiroho kwa wengine ambao hawashiriki imani yao. Karibu 3 kati ya vijana 3 kati ya 10 wanasema wanashirikisha mambo ya kiroho kwa mwezi au mara kwa mara, na vijana wa Kikristo hawaenezi injili zaidi ya wastani.

## KUWA NA MAZUNGUMZO YA KIROHO

*Ni kwa kiwango gani vijana hushirikisha mambo ya dini au ya kiroho kwa wengine ambao hawashiriki imani yao. (kila mwezi au mara kwa mara).*




Utafiti huu uligundua kuwa **44% ya vijana wa Kikristo** hawaamini kuwa wana jukumu la kushirikisha imani yao kwa wengine.

# Hitimisho

Ni muhimu kukumbuka kuwa taswira hii ya mtazamo na tabia za kidini za vijana ni picha tu. Tabia hizi hazijazama kwa undani kwenye maisha ya vijana na zinaweza kubadilika sana kadri wanavyokua. Lakini kwa sasa, utafiti huu unatupa mwanga kuhusu vijana na unatuelekeza kwenye matokeo halisi na jinsi tunavyoweza kuyatendea kazi.

- **WEKEZA KWENYE UTAYARI WA KIROHO WA KIZAZI HIKI.**
  Kizazi hiki kinaonesha utayari kwenye wazo la kuwa kiroho na wasioamini wengi wanasema wako tayari kuhudhuria kanisani. Kwa kuongezea, tayari wana mtazamo chanya juu ya Wakristo kuwa ni wakarimu na wanaojali. Mazungumzo yanayoanza na mtazamo kwamba wanadamu wamekusudiwa kuwa kiroho yanaweza kufungua milango kwenye uchunguzi wa kina wa imani.

- **KUMFUATA KRISTO NI UTAMBULISHO NA NIDHAMU.**
  Vijana wenye imani thabiti ya Kikristo na kuhusisha hilo na tabia ya kusoma maandiko na maombi wanaona tofauti kubwa maishani mwao kulinganisha na uhalisia wa maisha ya Wakristo wa Kawaida au vijana wengine. Kuandaa uanafunzi wa kizazi hiki kwa kulenga imani thabiti na desturi zaweza kuleta sehemu nyingi za maisha yao kwenye taratibu.


- **BAADHI YA KWELI ZAWEZA KUWA NA UPEKEE.**
  Vijana Wakristo katika utafiti huu wanaonekana kutokuwa tayari kujitoa kwa ajili ya ukweli wa kipekee au kuwajibika kuushirikisha ukweli huu kwa wengine. Je, tunawezaje kuwasaidia vijana waelewe upekee wa Injili na changamoto ya kuishi mkristo imara katikati ya tamaduni zinazohubiri uvumilivu na mjumuisho?




# UZOEFU NA MAHANGAIKO BINAFSI


# Tulichogundua

Idadi kubwa ya vijana wanahangaika na afya ya akili, upweke, msongo, fadhaa na mawazo ya kujaribu kujiua.



**1 kati ya vijana 4** wanaripoti kuwa ndani ya miezi mitatu iliyopita **wamekuwa na mawazo ya kujiua.**




**1 kati ya vijana 14** wanasema kuwa ndani ya miezi mitatu iliyopita **wamejaribu** kujiua.

**Wasichana wanahangaika** zaidi ya wavulana linapokuja suala la afya ya akili na **ni mara mbili zaidi kusema wamejaribu kujiua.**




VIJANA DUNIANI




**3 kati ya vijana 10** wanaripoti kuwa ndani ya miezi mitatu wamejihusisha na ngono.

WAKRISTO



Kuna kiwango **cha juu hata kati ya Wakristo** (1 kati 3).

*Angalizo: Hii linalenga vijana wasiooa*



**1 kati ya vijana 5** wanasema kuwa ndani ya miezi mitatu amevutiwa **kimapenzi na mtu wa jinsia yake.**


# *Kutazama kwa kina Afya ya Akili*

Ujana ni wakati wa maisha unaoweza kujawa na magumu kwenye ngazi mbali mbali. Vijana wanaweza kuhangaika kuwa wao ni nani na watakuwa nani; ni mahiri kwenye jambo gani na wanataka kufanya nini maishani; pasipo kuchunguza mahusiano ya kimapenzi na kujitafutia nafasi kwenye rika. Yapo mengine yanayoendelea kati ya vijana, na vijana katika utafiti huu walikuwa wazi kutueleza kuwa wanapitia baadhi ya mambo magumu.

Karibia vijana 2 kati ya 3 walisema wanajihisi upweke, zaidi ya nusu walisema fadhaa kuu, karibia nusu walisema msongo.[1] Vijana walitoa taarifa juu ya uzoefu binafsi na mahangaiko waliyokumbana nayo ndani ya miezi mitatu ya maisha yao, kwa takwimu zilizokusanywa ndani ya Februari-Machi 2020. Hii inamaanisha kuwa vijana walikuwa wanatafakari maisha kabla ya janga la korona lililopelekea kusitishwa kwa shughuli nyingi na kuwekwa karantini.

## AFYA YA AKILI DUNIANI

*Ndani ya miezi mitatu, Nimepitia:*





*1 Angalizo: Haya sio lazima yawe kwenye viwango vya kitabibu vya msongo au fadhaa. Vijana walijitafsiria wenyewe misamiati waliyopewa na kutoa taarifa yao binafsi kama walihisi walishakumbana nayo.*

Pia tuliwauliza vijana kutoa taarifa binafsi kama, ndani ya miezi mitatu iliyopita, walikutana na mawazo ya kujiua au walijaribu kujiua.

Mmoja kati ya wanne duniani kote walisema walishakumbana na mawazo ya kujiua, viwango vya nchi nne vikiwa 1 kati ya 3 au zaidi. Mawazo ya kutaka kujiua yanaweza kuwa na sura ya wazo la kawaida au la mbali hadi kuwa la kina na lenye mikakati.

> 1 KATI YA VIJANA 4 DUNIANI WALISEMA KUWA NA MAWAZO YA KUJIUA.


## NCHI ZINAZOONGOZA




Hata hivyo, sio mawazo yote ya kujiua yanakuwa majaribio ya kujiua. Ni 7% ya vijana Duniani (1 kati 14) walioripoti hilo ndani ya miezi mitatu iliyopita, nchi nne zilizoripoti kiwango cha juu kuliko 1 kwa 10.[1]

Ugunduzi katika utafiti huu juu ya majaribio ya kujiua kati ya vijana ni kuwa vijana ni rahisi zaidi kutoa taarifa zao kuliko watu wazima.

## MAJARIBIO YA KUJIUA KWA UMRI





*1 Ni muhimu kukumbuka kuwa takwimu hizi zimetolewa na vijana binafsi, hazikutolewa kwenye takwimu za hospitali au matukio ya nchi ambayo ndiyo msingi wa tafiti zingine kuhusu mada hii.*

# Vijana Wapo Gizani

Machapisho ya utafiti huu juu ya mada hii yanatupa vigezo kadhaa vinavyohusiana na hatari za vijana kuhusu kujiua ikiwa ni pamoja na mambo ya Ushoga, Ulawiti, Wanaotamani Jinsia zote, Kujibadili Jinsia na wenye Maswali juu ya Jinsia zao (LGBTQ); kutumia vilevi, kuoneana, na dalili za fadhaa na msongo.[1] Utafiti wetu uligundua kuwa pana muunganiko unaofanana. Vijana wanaohangaika juu ya utambulisho kijinsia, au mvuto wa kimapenzi ya jinsia moja wako kwenye hatari kubwa ya kujiua, sambamba na vijana wanaopitia manyanyaso mtandaoni na wale wanaopambana na matatizo ya kiakili. Matumizi ya pombe na madawa ya kujiliwaza yalionekana kusaidia kupandisha kiwango cha mawazo na majaribio ya kutaka kujiua.

## MAMBO 7 YANAYOHUSIANA NA KIWANGO HATARISHI CHA KUJIUA





Majaribio ya kujiua, kama mawazo ya kutaka kujiua, yanaangukia kwenye mwendelezo wa tabia hovyo zinazodhihirisha kutothamini maisha hadi mpango kamili wenye lengo la kujiua. Sio tukio moja linalopelekea vijana kujaribu kujiua, lakini yaweza kuwa mtiririko wa hatua ndogondogo na mawazo yanayojijenga juu ya mengine. Baadhi ya majaribio vijana waliyotolea taarifa kwenye utafiti wetu yanaweza yasiwe na umakini wa kuhitaji uangalizi wa kitabibu.

Pasipo kulenga moja kwa moja mazingira fulani, takwimu hizi zinatuonesha kuwa baadhi ya vijana wako kwenye giza linalowapeleka kwenye kukata tamaa. Takwimu hizi zinatupa sababu ya kutulia na kutafakari juu ya hali halisi na kuenea kwa kasi kwa hali hii kati ya maisha ya vijana. Linapokuja suala la kujiua, hatuangalia idadi kwenye kurasa au asilimia ya sampuli—lakini maisha halisi ya watu. Hii ina maana kuwa idadi yoyote ile ni kubwa sana.

*1 CDC WONDER Kanzidata Mtandaoni, Sababu zinazopelekea Vifo, Mafaili ya Sababu Kadhaa za Vifo 2015-2017. AmericasHealthRankings.org, Zilinukuliwa 2020.*

## WASICHANA WANAHANGAIKA ZAIDI

Wasichana wanahangaika zaidi kuliko vijana wa kiume kwenye mtazamo wao wa afya ya akili. Inawezekana kuwa wasichana wanajisikia huru zaidi kupaza sauti zao juu ya mahangaiko wanayopitia. Hata hivyo, imeonekana tofauti kubwa kati ya wasichana na wavulana kwenye maeneo na dini tofauti.





Imedhihirika kwamba kuwa Mkristo Imara hakubadilishi mambo hapa. Viwango vya mahangaiko binafsi vilionekana kuwa chini kati ya Wakristo Imara, lakini pengo kubwa lilibakia kati ya wavulana na wasichana kwenye kila kipengele.

# *Vijana na Ujinsia*

Miaka ya ujana inaweza kuwa wakati wa kujaribu ngono. Duniani, vijana 3 kati ya 10 walisema walishajihusisha na ngono ndani ya miezi mitatu iliyopita. Hii inaweza kuwakilisha upana wa tabia zenye athari, lakini katika kujibu hili swali vijana walijitafsiria wenyewe maana ya kujihusisha na ngono. Vijana wowote waliosema wameoana waliondolewa ili kuhakikisha kuwa takwimi hizi zinahusisha tu ngono nje ya muktadha wa ndoa. Vijana wa Ki-Afrika walionekana kujihusisha kwa kiwango kikubwa na ngono ilihali vijana wa Asia kiwango chao kilikuwa chini.


## KUJIHUSISHA NA NGONO KWA NCHI



# KUJIHUSISHA NA NGONO KWA UMRI


Kujihusisha na ngono ni mara tatu zaidi kati ya vijana wakubwa (18-19) Kulinganisha na Vijana wadogo (13-15).

Hata hivyo, zaidi ya kijana 1 kati 10 chini ya umri wa miaka 16 walisema wamejihusisha na ngono hivi karibuni. Viwango vilikuwa juu kati ya Wakristo wa Kawaida kwa kila umri. Wavulana na wasichana walikuwa karibia sawa kusema wamejihusisha na ngono.





# VIJANA WA KIKRISTO WAITIKIA

Kujihusisha na ngono kunaonekana kuwa tabia ambayo vijana hujihusisha nayo na kujitenga na msimamo wa maadili walionao kuhusu mada hiyo. Wakristo wana uwezekano zaidi kusema wamejihusisha na ngono karibuni kuliko vijana wa dini zingine. Ingawa wanathibitisha kuwa ngono ipo kwa ajili ya wanandoa, Vijana Wakristo Imara wanawezekana kujihusisha na ngono kama walivyo Wakristo wa Kawaida.




# JE, NI SAWA KUFANYA NGONO KABLA YA NDOA?



# *Picha za Ngono Ni Tatizo Halisi*


Takriban nusu (48%) ya vijana walikubali kuwa wametazama picha za ngono.

Wavulana ni zaidi sana kuliko wasichana kutazama mambo ya ngono ndani ya miezi 3 iliyopita (56% kwa 40%).

Kuna mtiririko wa takwimu kwa umri, vijana wakubwa walitazama picha za ngono zaidi kuliko vijana wadogo. Lakini kuwa mdogo haimaanishi kuwa umekingwa na hili. Kwa vijana wa miaka 13-15, 2 kati ya 5 walisema wametazama picha za ngono karibuni.

48% YA VIJANA WALISEMA WAMETAZAMA PICHA ZA NGONO.

## UTUMIAJI WA PICHA ZA NGONO KWA UMRI




## VIJANA WAKRISTO WAITIKIA



# HITIMISHO

Mahangaiko waliyoonesha vijana yanapaswa kutugusa. Hali ya kila kijana ni tofauti, na hakuna jibu moja kwa changamoto wanazokumbana nazo. Lakini ni muhimu tufahamu mambo yalivyo na unyeti wa aina ya maisha halisi vijana wanakabiliana nayo. Haya ni baadhi ya mambo ya ziada ya kufikiria tunapoondoka kwenye huruma hadi matendo:

- **WAKRISTO WANAHITAJI MALEZI KWENYE ENEO LA UJINSIA.**
  Vijana wengi leo wanatenga ngono kutoka kwenye muktadha wa ndoa takatifu na kuifanya kama tendo la kawaida la mtu kujifurahisha. Wakristo Imara walidhihirisha kuwa na uelewa kuwa ngono kabla ya ndoa ni mbaya, lakini ushawishi wa kimaadili waliyonayo haviwazuii kutojihusisha kwenye ngono. Haitoshi tu kuwafundisha vijana Biblia inachosema. Tutawezaje kuwaongoza vijana kuishi maisha ya ki-Biblia yanayothamini maadili na uwakili wa zawadi ya ujinsia?

- **MATUMIZI YA PICHA ZA NGONGO NI SUALA KUBWA KWA KIZAZI HIKI.**
  Takwimu zinaonesha kuwa hatuwezi kudhania kuwa umri au dini vitawalinda vijana kutotazama picha za ngono. Hata vijana wanaoshikilia Imani na nidhamu ya Kikristo bado wanahangaika kwenye eneo hili.

- **WASICHANA WANAWEZA KUHITAJI MSAADA ZAIDI.**
  Tofauti ya mahangaiko binafsi kijinsia haipingiki; na viwango vya juu kati ya wasichana havipuuziliki. Kuwa Mkristo Imara kuna msaada wa jumla, lakini hakuzibi pengo kati ya jinsia. Fikiria upekee wa mahangaiko wasichana wanayopitia na jinsi tunavyoweza kuwawezesha wanawake walioimarika kukilea kizazi hiki.




# MUUNGANIKO WA KIDIJITALI NA MATOKEO YAKE


# Tulichogundua




Kwa wastani vijana **wanatumia saa 7 na da-kika 23** kwenye mtandao kila siku.





ya vijana wanasema **wanatazama video kila siku.**




Vijana ambao ni **watumiaji wakuu wa** (saa 10+) **wanahangaika zaidi na afya zao za akili.**



Vijana wengi wanasema mitandao ya **kijamii Inachangia wao kupata ridhiko la maisha.**

**64%** ya vijana wanatumia mitandao ya kijamii kwa **saa moja au chini kidogo kila siku.**




# Muda Unaotumika Mtandaoni

Hiki ni kizazi kilichounganishwa kidijitali zaidi kuliko dunia ilivyowahi kuona. Vijana leo wanakua kwenye Intaneti, wana simu janja mikononi mwao kutoka umri mdogo, na hawajawahi kuufahamu ulimwengu usio na mitandao ya kijamii.

Kuwa na muunganiko wa Intaneti ilikuwa lazima kwenye utafiti huu. Moja ya malengo ya awali ya utafiti huu ulikuwa kuchunguza madhara ya muunganiko wa vijana kidijitali kuhusiana na mitazamo, imani na tabia.

Ni muda kiasi gani vijana wanatumia mtandaoni? Wanafanya nini wakiwa mtandaoni? Je, matumizi ya teknolojia yanashawishi vipi mambo mengi kwenye maisha yao? Haya yalikuwa baadhi ya maswali tuliyoyagusia kwenye utafiti huu.

Vijana wanatumia kwa wastani saa 7 na dakika 23 kwenye mtandao kwenye nchi 20 zilizofanyiwa utafiti. Vijana wa Brazili wanakaa muda zaidi mtandaoni karibia saa 9.5 kila siku, wakati vijana China wanakaa muda kidogo zaidi mtandaoni saa 5.5.




| | NCHI |
|---|---|
| 9:29 | Brazili |
| 9:07 | Indonesia |
| 8:29 | Argentina |
| 8:28 | Nigeria |
| 7:54 | Urusi |
| 7:40 | Kenya |
| 7:35 | Marekani |
| 7:34 | India |
| 7:22 | Mexico |
| 7:22 | Afrika Kusini |
| 7:19 | Colombia |
| 7:19 | Uingereza |
| 7:08 | Ureno |
| 6:50 | Vietnam |
| 6:45 | Hispania |
| 6:43 | Misri |
| 6:42 | Uholanzi |
| 6:29 | Romania |
| 6:03 | Japani |
| 5:24 | China |


VIJANA WANATUMIA ZAIDI YA SAA 7 MTANDAONI KILA SIKU



# *Yanayofanyika Mtandaoni*

Vijana wanafanya nini saa zote hizo kwenye mtandao? Vijana wanasema wanatumia muda zaidi kuongea, kutumiana arafa, au kuchati kwenye video. Mitandao ya kijamii inagharimu saa nyingi zaidi, ikifuatiwa na kutazama video au filamu, na mwishowe michezo.

## MUDA UNAOTUMIKA KWA SHUGHULI MOJA DUNIANI




## NCHI ZINAZOONGOZA

Vijana kwenye baadhi ya nchi hutumia muda zaidi kuliko wastani wa Dunia kwenye kila shughuli.

**kuchati**
KENYA 3:45

**mitandao ya kijamii**
NIGERIA 4:00

**kutazama video**
MAREKANI

**michezo**
ARGENTINA 2:38

Jumla ya muda uliotumika sio njia pekee ya kupima vijana wanachofurahia. Aina ya shughuli wanazofanya kila wakati kunajenga taswira ya uhusika wao kidijitali. Shughuli maarufu kila siku kati ya vijana ni kutazama video.

Asilimia tisini na nne ya vijana walisema wanatazama video kila siku. Shughuli ya pili maarufu zaidi ni mitandao ya kijamii. Karibia vijana wote wanatumia mitandao ya kijamii kila siku, hata hivyo 64% wanatumia saa moja au chini yake kwenye majukwaa haya.


Vijana walikuwa na majibu mchanganyiko kwenye mitandao kwa ujumla. Wengi wanakubali uwepo chanya, vijana watatu kati ya watano wanakubali kuwa mitandao ya kijamii inawasaidia kupata ridhiko la maisha.

Hata hivyo, zaidi ya nusu ya vijana walisema wakati mwingine au mara nyingi wanajisikia huzuni, fadhaa au msongo.

**94%** ya vijana hutazama video kila siku.

**64%** wanatumia saa moja au chini yake kwenye mitandao ya kijamii.

## MITANDAO YA KIJAMII HUNIFANYA NIJISIKIE HUZUNI, FADHAA, AU MSONGO




# Ushawishi wa Intaneti

Tulipokea majibu tofauti tofauti kutoka kwa vijana kuhusu mazoea na muda wanaotumia mtandaoni, likatufanya kugawanya vijana kwenye makundi ya watumiaji wadogo wa intaneti (saa 0-4 mtandaoni kila siku) na watumiaji wakuu (saa 10+ mtandaoni kila siku). Kwa kuzitazama takwimu hizi kwa lensi hii kunadhihirisha matokeo ya kushangaza.

Inahusiana na malengo ya maisha, vijana ambao ni watumiaji wakuu wa intaneti wanaonekana kuwa na mtazamo wa kiujasiriamali na utafutaji hela kwenye malengo yao ya maisha kuliko watumiaji wadogo wa intaneti. Vijana pia wanaonesha utofauti kwenye mambo ya kifamilia. Watumiaji wakuu wa intaneti wanaonekana kutokuwa na mguso mzuri wa kifamilia, na pia wana uwezekano zaidi kusema kuwa kwa nadra au hawajawahi kuzungumza na wazazi wao kuhusiana na mambo muhimu maishani mwao.

## MATUMIZI YA INTANETI NA UZOEFU MAISHANI




Mwelekeo wa takwimu zinazoonesha kuwa muunganiko ulenga kwenye mitazamo na maoni fulani. Kwa mfano, vijana watumiaji wakuu ni wepesi zaidi kusema kuwa ni sawa kufanya ngono kabla ya ndoa na kuwa inakubalika kubadilisha mwili wako kuwa jinsia tofauti. Baadhi ya haya hayashangazi, labda, kwa kuwa vijana wanatumia muda mwingi mtandaoni wakijihusisha na mtazamo mpana wa dunia kuhusu maadili.

## MATUMIZI YA INTANETI NA MAHANGAIKO BINAFSI

**WATUMIAJI WADOGO WA INTANETI** *(saa 0-4 kwenye mtandao kila siku)*

**WATUMIAJI WAKUBWA WA INTANETI** *(saa 10+ kwenye mtandao kila siku)*

*Ndani ya miezi mitatu iliyopita nimekutana na:*




Baadhi ya uhusiano wa kushangaza kwenye takwimu ulijitokeza wakati matumizi ya intaneti kwa vijana yaliposhabihiana na uhalisia wa maisha wanayoishi. Watumiaji wakubwa wa intaneti wanaonekana kuhangaika zaidi na matatizo ya afya ya akili. Vijana wanaotumia saa 10 au zaidi kwenye mtandao kila siku wanaripoti kiwango kikubwa cha fadhaa na msongo kulinganisha na watumiaji wadogo wa intaneti. Ni mara mbili zaidi kujielezea kuwa ndani ya miezi mitatu iliyopita walishajaribu kujiua.

Kwa hakika, matokeo haya yanagusa sana. Hata hivyo, uhalisia wa uhusiano kati ya muda wa mtandao na mahangaiko binafsi ya vijana vinatofautiana sana. Takwimu hizi zinaonesha kuwa kuna aina fulani ya muunganiko kati yake, lakini haimaanishi kuwa kimoja kinasababisha kingine. Inawezekana kuwa vijana watumiaji wakuu wa intaneti wanadhihirisha hisia za kukosa matumaini kwenye maisha yao. Kwa upande mwingine, vijana ambao tayari wanahangaika na afya ya akili wanaweza kuvigeukia vifaa vyao vya kidijitali kama njia ya kukwepa tatizo hilo. Yote yanaweza kuwa sahihi kwa kiasi fulani.

# Hitimisho

Hatuwezi kusahau kuwa miaka ya ujana inaweza kujawa na mabadiliko ya homoni, vurugu za kijamii na usumbufu mwingine vinavyoweza kuchangia hali dhaifu ya afya ya akili. Muda unaotumika kwenye vifaa vya kidijitali ni kipengele kimoja tu kati ya vingi vinavyoathiri maisha na uzoefu binafsi wa vijana leo. Haya yote yana maana gani kwa jinsi tunavyojihusisha na kizazi hiki kilichounganishwa kidijitali? Haya ni baadhi ya mawazo ya kufikiria:

- **VIDEO NI MAARUFU SANA KATI YA VIJANA.**
  Ni njia yenye nguvu sana ya kuwafikia vijana. Kumbuka, 94% ya vijana wanajihusisha na video kila siku. Tunawezaje kutumia njia hii yenye ushawishi kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo?


- **MITANDAO YA KIJAMII INALETA MIITIKIO TOFAUTI.**
  Vijana wengi hutazama matukio kwenye mitandao yao ya kijamii, lakini hatumii muda mwingi huko (64% hutumia saa 1 au chini yake kila siku). Kwa kuongezea, vijana wamegawanyika juu ya iwapo mitandao ya kijamii inawasaidia au inawaharibu. Tunawezaje kukisaidia kizazi hiki kuchambua madhara ya tabia zao za kidijitali na kupambanua magumu wanayopitia?

- **VIJANA KWA UPANDE MWINGINE WANAWEZA KUWA WANAHANGAIKA SANA.**
  Wale wanaotumia muda mwingi mtandaoni wana uwezekano zaidi kusumbuliwa na matatizo ya afya ya akili, hivyo fikiria jinsi ambavyo unaweza kujiandaa kwa mazungumzo yanayoweza kuibuka.




# UTAMBULISHO NA MAHUSIANO

# Tulichogundua



Karibia nusu ya vijana wanaamini kuwa **jinsia imejikita zaidi kwenye ile ambayo mtu amezaliwa nayo.**




Nusu nyingine wanaamini ni kitu **mtu anachojiamulia mwenyewe kulingana na hisia au mvuto wa kimapenzi.**





**Wasichana** wana **mtazamo mdogo** wa kitamaduni juu ya ndoa kuliko wavulana.





**48%** ya vijana dunia wanaamini ndoa **zisiwe tu kati ya mwanaume na mwanamke.**



**1 kati 10** ya vijana wote wanashikilia **mtazamo wa kimaandiko** kuhusu ndoa.




**Vijana wanaridhika na mahusiano yao, 82%** wakidai **kuwa mahusiano na familia zao ni mzuri** na idadi hiyo hiyo wakisema **wana marafiki wa karibu wanaowafahamu vizuri.**

# *Utambulisho wa Kijinsia Kama Uchaguzi*

Utambulisho wa kijana na mahusiano yake ni mambo nyeti mno na ya kibinafsi. Hakuna utafiti unaoweza kupima kila jambo, hivyo tulichagua kulenga maeneo kadhaa muhimu kuona namna ambavyo vijana wanavyojiona wenyewe na wanavyoona wengine. Wanasema nini kuhusu utambulisho wa kijinsia na hilo lina maana gani kwao? Ni kwa kiwango gani wanaridhishwa na mahusiano walionayo na marafiki na familia zao? Ni mtazamo gani wanaoenda nao kwenye utu uzima juu ya mada kama ngono na ndoa? Mazungumzo haya ni magumu, lakini hapa tuangazie tuliyogundua kwenye haya maeneo muhimu.


Karibia nusu ya vijana duniani wanashikilia mtazamo wa kitamaduni kuhusu jinsia, wakisema kuwa jinsia imejikita zaidi kwenye hali ambayo mtu amezaliwa nayo. Lakini nusu nyingine wanaamini jinsia ni uchaguzi— ni kitu cha kujiamulia binafsi kulingana na hisia au mvuto wa kimapenzi. Hili ni kundi kubwa la vijana wanaoamini kuwa jinsia haina msimamo thabiti, bali unaotegemeana na mtu.

## JINSIA IMEJIKITA ZAIDI KWENYE





Vijana wengi pia wanaamini kuwa kama mtu akijisikia kuwa wa jinsia tofauti, basi aweze kufanya jambo kuhusiana na hilo.

Wawili kati ya vijana watano duniani wanasema inakubalika kwa mtu kubadilisha mwili wake kuwa jinsia tofauti.




## MTAZAMO WA JINSIA KWA ENEO




Maoni ya kizazi hiki juu ya jinsia yanatofautiana kwa kiasi kikubwa kulingana na eneo la dunia wanakotoka. Amerika ya Kusini kwa mfano, idadi ya vijana wanaochukulia jinsia kuwa kitu cha kujiamulia binafsi ni karibia mara mbili ya wale vijana wanaoamini kuwa jinsia mtu anazaliwa nayo. Kinyume chake, vijana wengi Afrika hawaoni jinsia kama kitu cha kujiamulia. Takribani 3 kati ya vijana 4 kwenye nchi za Afrika huamini kuwa jinsia ni ile ambayo mtu amezaliwa nayo.

## UTAMBULISHO WA KIJINSIA NA MABADILIKO




Wakati vijana wengi wakikubaliana na dhana ya kuwa masuala ya jinsia ni matakwa binafsi, utafiti wetu ulituonesha idadi ndogo ya vijana wanaosema kuwa binafsi wanachanganyikiwa juu ya utambulisho wao wa kijinsia au wana shauku ya kubadilisha jinsia zao.


Asilimia kumi ya vijana duniani wanasema kuwa ndani ya miezi 3, wamepitia kuchanganyikiwa juu ya utambulisho wao wa kijinsia, na 15% wanasema wanajisikia kutaka kuwa jinsia tofauti. Wasichana wako juu kidogo ya wavulana kusema wanahangaika na utambulisho wao wa kijinsia (12% kwa 9%), na cha kufurahisha ni kuwa kiujumla wana mtazamo tofauti kuliko wavulana juu ya mada hii. Wengi wa wasichana (59%) wanaamini kuwa jinsia imejikita zaidi kwenye hisia au shauku ya mtu binafsi kulinganisha na wavulana wachache (42%) wanaosema hivyo. Wasichana pia wana uwezekano mkubwa zaidi kusema kuwa ni sawa kwa mtu kubadilisha jinsia yake kuwa mtu wa jinsia tofauti (52% kwa 32%).

# *Ushawishi wa Dini*

Dini ya kijana ni kipengele kingine chenye athari wazi juu ya maoni yake kuhusiana na utambulisho wa kijinsia. Kati ya dini zote, Waislamu wanashikilia zaidi mtazamo uliozoeleka kuhusu jinsia. Asilimia sitini na mbili ya vijana wa Kiislamu wanasema kuwa jinsia ni ile uliyozaliwa nayo, ikifuatiwa na 50% ya Wakristo, na 41% ya vijana wa dini zingine. Vijana wanaosema hawana dini wanaongoza katika kuamini kuwa jinsia ni uamuzi binafsi wa jinsi mtu anavyojisikia au mvuto wa kimapenzi alionao (63%).

Hata hivyo, mtazamo ni tofauti sana kati vijana Wakristo Imara ambao wanashikilia imani thabiti na wanaosema wanatabia ya kusoma Biblia na kuomba. Saba kati ya kumi ya vijana Wakristo Imara wanashikilia mtazamo uliozoeleka kuhusu jinsia, na ni 1 kati ya 10 wanaoamini kuwa kubadilisha jinsia ni kitu kinachokubalika.


## VIJANA WAKRISTO WANAITIKIA




# *Mvuto wa Mapenzi ya Jinsia Moja*

Idadi kubwa ya vijana wanasema kuwa mvuto wa mapenzi ya jinsia moja ni kitu ambacho wamekumbana nacho. 1 kati ya vijana 5 duniani wanasema kuwa walishajisikia kuvutiwa kimapenzi na mtu wa jinsia yake ndani ya miezi mitatu iliyopita. Wakristo wa Kawaida ni wepesi zaidi kusema hivyo kuliko Wakristo Imara.

1 KATI YA VIJANA 5 DUNIANI WANARIPOTI KUVUTIWA NA MAPENZI YA JINSIA MOJA



## MVUTO WA MAPENZI YA JINSIA MOJA KWA NCHI





Katika kutafiti mada hii sawa na vipengele vingine kwenye utafiti, uligundulika muunganiko wa kushangaza. Kwa mfano, wasichana ni mara mbili zaidi kuvutiwa na mapenzi ya jinsia moja kuliko wavulana (28% kati ya 13%). Mambo anayokutana nayo nyumbani pia yanaonekana kuchangia. Vijana wanaosema kuwa na mahusiano dhaifu ya kifamilia wanasukumwa zaidi kwenye mapenzi ya jinsia moja kuliko wale wenye mahusiano mazuri kwenye familia (30% kwa 18%).


Dini inaonekana kuwa kipengele chenye suluhu. Vijana wanaojitambulisha kuwa na dini yoyote ile wana kiwango cha chini katika kusema wanavutiwa na jinsia moja kulinganisha na vijana wanaosema hawana dini (18% kwa 25%). Mvuto wa mapenzi ya jinsia moja uko chini sana kati ya Waislamu (13%) Wakristo Imara (12%).

Hatimaye, mvuto wa mapenzi ya jinsia moja unaonekana kuwa kundi moja na tabia zingine. Kwa vijana wanaripoti kujaribu kujiua hivi karibuni, karibia nusu (46%) pia wanasema wamevutiwa na mapenzi ya jinsia moja. Matumizi ya madawa ya kulevya, msongo, fadhaa kuu, au kutazama picha za ngono ni mambo ambayo yanazidisha mara mbili uwezekano wa mvuto wa mapenzi ya jinsia moja.

## MAMBO 4 YANAYOHUSIANA NA MVUTO WA MAPENZI YA JINSIA MOJA



# Mtazamo wa Ndoa




Tulipima pia maoni ya vijana juu ya ndoa—mtazamo watakwenda nao kwenye utu-zima na kwenye mahusiano yao ya baadaye.

Vijana wengi (57%) wanaamini kuwa ndoa ni jambo la kudumu maishani, lakini kiasi fulani hawana uhakika (27%) au hawakubaliani na hoja hiyo (16%). Vijana hawashawishiki kuwa ndoa zinapaswa kuwa tu kati ya mume na mke. Nusu nzima (48%) ya vijana wanasema hapana, wakati wachache (40%) wanasema ndio.


Cha kushangaza, wasichana wana mtazamo tofauti juu ya ndoa kuliko wavulana. Kwa wastani, wasichana hawashawishiki kuwa ndoa inapaswa tu kuwa jambo la kudumu maishani (53% kwa 61%) na wana uwezekano kusema kuwa sio lazima iwe kati ya mwanaume na mwanamke (58% kwa 38%).

Kwa kutazama maoni kwenye tamaduni mbali mbali, vijana wana mwitikio tofauti. Vijana wa Afrika wanaamini zaidi kuwa ndoa ni jambo la kudumu maishani, wakati wa Amerika ya Kusini wanaangukia upande wa pili wa shilingi.

Mtazamo wa Biblia kuhusu ndoa ni maoni ya wachache. Ni 1 kati ya vijana 7 wanaoamini kuwa ndoa iwe jambo la kudumu kati ya mwanaume na mwanamke, na kwamba ngono iwe tu kwa wanandoa.


1 KATI YA VIJANA 7 WANA MTAZAMO WA BIBLIA JUU YA NDOA

## VIJANA WAKRISTO WAITIKIA




Tofauti na mafundisho ya Biblia juu ya mada hii, Wakristo wanaendana na wastani wa dunia (51%) kuamini kuwa ngono kabla ya ndoa inakubadilika. Vijana Wakristo wao ndio rahisi zaidi kuliko dini zingine kusema kuwa ndani ya miezi 3 wamejihusisha na ngono (34% kwa 26%).

Wakristo Imara wana mtazamo wa Biblia zaidi juu ya mada hizi, hata hivyo wanaripoti kujihusisha na ngono hivi karibuni.




# *Marafiki na Mahusiano ya Familia*

Linapofikia suala la jamii yao ya sasa, vijana wengi wanaridhika na mahusiano walionayo na marafiki na familia zao. 82% ya vijana duniani wanasema kuwa mahusiano na familia zao yamekuwa mazuri. Hiki ni kiwango kikubwa kwa kuzingatia upana wa familia, tamaduni, na mazingira yaliyowakilishwa kwenye utafiti.



**57% ya vijana wanaishi kwenye kaya yenye wazazi wawili.**




**35% wanasema wanaishi na mzazi mmoja au ndugu wa familia.**

India ndio nchi pekee kwenye utafiti wetu ambapo hizi takwimu zilibadilishwa. Karibia nusu (47%) ya vijana India walisema wanaishi na mzazi mmoja, na 20% wanaishi na wazazi wote wawili. Hata hivyo, vijana wa India walionesha kuridhika na mahusiano ya familia zao kulinganisha na nchi 20 kwenye utafiti wetu. Idadi kubwa 93% ya vijana wa India wanasema mahusiano yao na familia zao yamekuwa mazuri.

Pia tulikusanya baadhi ya taarifa muhimu zinazotuonesha ukaribu wa vijana na wazazi wao kwa kuwauliza jinsi mazungumzo juu ya mambo muhimu ulivyo. Wengi wa vijana duniani wanasema kwa nadra au mara kwa mara huzungumza na wazazi wao juu ya mambo yenye umuhimu kwao.






**81% ya vijana duniani wana-sema kuwa wakati mwingine au mara zote huzungumza na wazazi wao kuhusu mambo yenye umuhimu kwao.**

**1 kati vijana 5 wanasema kuwa kwa nadra au hawafanyi hivyo.**


Kwa mara nyingine, India imekuwa nchi iliyoibuka kwa 63% ya vijana kusema kuwa wanazungumza na wazazi wao kuhusu mambo yenye umuhimu kwao.

Kwa upande mwingine wa shilingi, vijana wa Marekani ndio wenye kiwango cha chini katika kuzungumza na wazazi wao mara kwa mara. Marekani pia ipo kundi la chini kuhusiana na ridhiko la familia. Watatu kati ya vijana kumi wa Marekani walisema mahusiano yao na familia hayajawa mazuri kwa ujumla.




> 82% YA VIJANA DUNIANI WANASEMA WANA UHUSIANO WA KARIBU NA MARAFIKI WANAOWAFAHAMU VIZURI

## NINA MARAFIKI WA KARIBU WANAONIFAHAMU VIZURI




Vijana pia wanadhihirisha kuwa wana urafiki wenye nguvu maishani mwao. Asilimia themanini na mbili ya vijana duniani wanasema wana marafiki wa karibu wanaowafahamu vizuri. Idadi ndogo ya vijana hawakukubali hilo kwenye nchi chache tu duniani.

Cha kushangaza, dini na jinsia havionekani kuchukua nafasi kubwa kwenye utoshelevu wa vijana na marafiki au familia zao. Miitikio ilikuwa inafanana kati ya wavulana na wasichana na kati ya vijana wa dini tofauti kuhusiana na urafiki wa karibu, mahusiano mazuri na familia, iwapo au kuwa na mazungumzo yenye maana na wazazi wao.

# *Hitimisho*

Mada za utambulisho na mahusiano zinaweza kuwa na sura nyingi na ngumu kuzitatua. Kila mtu anabeba historia yake ya nyuma, uzoefu, na maoni yao kwenye mazungumzo. Ingawa hakuna mtazamo mmoja unaofafanua hiki kizazi duniani, takwimu zinadokeza mwenendo unaoibuka unavyoweza kusaidia uelewa na mwitikio wetu.

- **KIZAZI HIKI KIMEGAWANYIKA KWENYE MTAZAMO WAKE JUU YA UTAMBULISHO WA KIJINSIA.**
  Nusu ya vijana leo wanaamini kuwa jinsia ni ile mtu anayozaliwa nayo, wakati nusu nyingine wanasema ni kitu mtu binafsi anaweza kujiamulia kulingana na mtu binafsi anavyojisikia au mvuto wake kimapenzi. Je, tunawezaje kuwahusisha vijana kwenye mazungumzo kamili ya mada hii na matokeo ya maamuzi haya muhimu ya maisha?

- **VIJANA WANA MITAZAMO YAO WENYEWE JUU YA NDOA.**
  Kizazi hiki kinaonekana kuhama kutoka mtazamo uliozoeleka juu ya ndoa kama jambo la kudumu maishani kati ya mwanaume na mwanamke. Kwa kuongezea, wengi wa vijana hawaoni hitaji la kuachilia ngono kwa wanandoa. Tunawezaje kuwasaidia vijana sio tu kuelewa mpango wa Mungu juu ya ndoa, bali pia faida za kumaanisha linapokuwa suala la agano?

- **WASICHANA WANA MITAZAMO NA UZOEFU TOFAUTI KULIKO WAVULANA.**
  Utafiti huu unatuonesha kuwa wasichana wana mtazamo kidogo juu ya msimamo wa biblia kuhusu ndoa kuliko wavulana na ni wepesi zaidi kukumbana na mgogoro wa kijinsia. Takwimu zinatuonesha kinachoendelea, lakini sio kwanini ni kweli au ni nini kinachosababisha mwelekeo huu. Ni kwa jinsi gani tunaweza kuendana na wasichana ili kuwaelewa zaidi juu ya maoni, uzoefu, na mahangaiko walionayo kwenye maeneo haya?

- **VIJANA WANARIDHIKA KABISA NA MAHUSIANO YAO NA FAMILIA ZAO.**
  Ilifurahisha kuwaona vijana wa India wana furaha zaidi juu ya mahusiano na familia zao, ingawa wengi wao wanaishi na familia za mzazi mmoja. Hili linadokeza kuwa vijana wanazipenda familia zao hata pasipo kujali muundo wake au magumu wanayoweza kupitia kwenye safari.




# USHAWISHI NA SAUTI ZINAZOONGOZA

# Tulichogundua

## MAANA YA MAISHA

Vijana wanasema **familia** ndio msingi wa ushawishi unaongoza kwenye baadhi ya maswali muhimu kama nini ni sawa na kibaya na chenye maana maishani.







## JINSIA NA NGONO

**Mitandao ya kijamii** na marafiki ndio washawishi wakuu wa vijana kuhusiana na mazungumzo juu ya jinsia na ujinsia.

**Uzoefu binafsi** ni sababu namba moja ya vijana kusema kuwa **watabadilisha mawazo yao kuhusu imani ya dini.**



Kwa ulinganifu ni vijana wachache wa Kikristo wanaosema kuwa **mafundisho ya wachungaji** yamekuwa sababu ya msingi ya kubadilisha mawazo yao kuhusu imani ya dini.





Vijana **Wakristo Imara** ni mara nne zaidi **kuweza kuigeukia Biblia au wachungaji** wao kupata mwongozo kuliko vijana Wakristo wa kawaida.

# *Vishawishi na Sauti Ziongozazo*

Vijana wana maoni juu ya mambo mengi, lakini mawazo hayo kwa nadra yanajijenga pasipo ushawishi. Tulikuwa wadadisi kuhusu vishawishi vikuu vya kizazi hiki.

Ni nani wanayemwamini kwa mwongozo na ushauri? Linapokuja suala la baadhi ya mambo muhimu zaidi ya maisha, ni sauti zipi wanazisikiliza? Ni kitu gani kitabadilisha mawazo yao juu ya imani thabiti?

Ingawa si kwa utimilifu, takwimu hizi zinatupa mwanga fulani jinsi vijana wa leo wanavyojenga mitazamo yao.


## VIJANA WANAZIAMINI FAMILIA

Vijana wanatuambia kuwa wanazigeukia familia mara kwa mara kupata mwongozo juu ya mada muhimu kwenye maisha. Wanafamilia ndio washawishi wakuu linapokuja suala la maana ya maisha au nini chema au kibaya.

Marafiki au rika na mitandao ya jamii imeibuka kuwa kati ya vishawishi vikuu vitatu vya vijana, wakati waalimu au washauri, viongozi wa dini au maandiko, na vyombo vya habari visivyo vya mtandao kushika nafasi ya chini kwenye orodha ya vishawishi.

Kwa hakika kuna maeneo mengine mengi ambayo tungeweza kuwahoji vijana kuyahusu. Lakini unachoamini kuhusu kusudi kuu la maisha na msingi wa maadili unatoka wapi vina athari juu ya namna utakavyoenenda.

**MAANA YA MAZUNGUMZO**
JUU YA MAISHA



1. WANAFAMILIA **41%**
2. MTANDAONI / MITANDAO YA KIJAMII **20%**
3. MARAFIKI/ RIKA **19%**
4. WAALIMU / WASHAURI **7%**
5. VYOMBO VYA HABARI VISIVYO VYA MTANDAO **7%**
6. VIONGOZI WA DINI / MAANDIKO **7%**

## MAZUNGUMZO JUU YA
MEMA NA MABAYA

1. WANAFAMILIA **50%**
2. MARAFIKI/ RIKA **16%**
3. MTANDAONI / MITANDAO YA KIJAMII **14%**
4. WAALIMU / WASHAURI **9%**
5. VIONGOZI WA DINI / MAANDIKO **7%**
6. VYOMBO VYA HABARI VISIVYO VYA MTANDAO **5%**

Maswali haya mawili ya msingi yana umuhimu kote kwenye umri ambao vijana wanajenga mitazamo yao—seti ya miongozo ya imani—watakayokwenda nayo hadi utu-uzima.


Linapokuja suala la maadili, vijana wa Amerika ya Kusini wanaegemea zaidi kwenye familia kuliko eneo lingine la dunia. Watatu kati ya vijana watano wa Amerika ya Kusini wanasema familia ni mahali pa kwenda-kwa taarifa au mwongozo juu ya kilicho chema na kibaya.

Lakini hata katika nchi ambazo kiwango cha makubaliano kilikuwa chini, familia ilibakia kuwa jibu la juu kwa waliojibu.

## USHAWISHI WA FAMILIA KWA NCHI

*Naiendea familia mara nyingi kwa taarifa au mwongozo juu ya kilicho chema na kibaya:*

**NCHI ZINAZOONGOZA** | **NCHI ZENYE KIWANGO CHA CHINI**




Familia inabakia kuwa sauti muhimu inayoongoza vijana hata katika nchi ambazo vijana wanasema wana mahusiano mabaya na familia zao. Kwa mfano, Marekani ni nchi iliyopo kundi la chini kuhusiana na vijana kuridhika na familia zao. Hata hivyo, vijana wa Marekani wana kiwango cha juu ya wastani kusema kuwa wanazigeukia familia zao mara nyingi kwa ushauri au mwongozo juu ya kilicho chema na kibaya (52%) au maana ya maisha (42%). Inaonekana kuwa pamoja na vikwazo kwenye safari, wazazi na wanafamilia wanaendelea kuwa ushawishi uliotukuka kwenye maisha ya vijana.

Labda cha kushangaza, ushawishi wa vijana unaonekana kuwa tofauti kulingana na dini zao. Wakristo ni wepesi zaidi kuliko vijana wengine kuzigeukia familia zao kupata mwongozo kuhusu maana ya maisha, na chini kidogo kugeukia mitandao ya kijamii au marafiki na rika.

Wachache kuliko kijana 1 kwa 10 Wakristo walisema wanawaendea wachungaji au Biblia zao zaidi kupata mwongozo juu ya maana ya maisha.

## USHAWISHI KWA DINI

*Naenda Wapi mara nyingi kwa ushauri au mwongozo wa maana ya maisha:*




# *Mazungumzo Tofauti*

Eneo lingine tulilowauliza vijana lilihusu mada kama jinsia, ujinsia, na mambo ya mapenzi. Mazungumzo haya yanaonekana kuwa tofauti huku vijana wakiripoti ushawishi tofauti.

Intaneti ni sauti yenye mwongozo hapa, zaidi ya kijana 1 kati ya vijana 3 wanasema wanageukia mitandao ya kijamii mara nyingi kupata taarifa au mwongozo juu ya mada hizi. Marafiki au rika wanakuwa ushawishi wa pili, na wanafamilia wakiwa wa tatu. Viongozi wa dini au maandikio yanaangukia chini kabisa ya orodha.

Hata kati ya Wakristo, vyanzo vya mtandaoni au mitandao ya kijamii vinaiweka kando familia kama kishawishi kikuu kwenye mada hizi. Linapokuja suala la jinsia na ujinsia, sauti ya utamaduni inaonekana kuzamisha sauti zingine kama Maandiko au kanisa.


**MAZUNGUMZO YA**
JINSIA NA UJINSIA



1. MTANDAONI / MITANDAO YA KIJAMII **36%**
2. MARAFIKI / RIKA **23%**
3. WANAFAMILIA **20%**
4. WAALIMU / WASHAURI **11%**
5. VYOMBO VYA HABARI VISIYO VYA MTANDAO **6%**
6. VIONGOZI WA DINI/ MAANDIKO **4%**

Hata hivyo, tunaona tofauti kubwa kati ya Wakristo Imara wanaoshikilia misingi thabiti ya Ukristo na wenye tabia ya kusoma Biblia na kuomba. Vijana hawa wanasikiliza zaidi viongozi wao wa dini na Neno la Mungu. Vijana Wakristo Imara ni mara nne zaidi kuliko Wakristo wa Kawaida kusema wanakwenda mara nyingi kwa viongozi wao wa dini au maandiko kupata mwongozo.

**WANAKWENDA KWA VIONGOZI WA DINI AU MAANDIKO MARA NYINGI KUPATA TAARIFA AU MWONGOZO**




# *Ni Nini Kingebadilisha Mawazo Yao*

Ushawishi unaweza kutusaidia katika kutupatia taarifa na maoni, lakini mwisho wa siku kila mtu anajiamulia atakachoamini na jinsi atakavyoshikilia imani hiyo.

Tulitaka kuchimba chini zaidi kutafuta kitakachowafanya vijana kubadilisha mawazo yao juu ya imani ya dini waliyonayo.

Uzoefu binafsi, kama jibu la maombi, lilikuwa jibu lililochaguliwa na wengi. Vijana walipendelea pia kuchunguza mambo wao wenyewe kuliko kuwaendea watu. Mazungumzo na watu wenye mamlaka kama wazazi au wachungaji yalishika nafasi ya chini kwenye orodha wakati mazungumzo na marafiki vilishika mkia.

NI KITU GANI KINAWEZA KUBADILISHA MAWAZO YAKO JUU YA IMANI YA DINI?




1. UZOEFU BINAFSI, KAMA JIBU LA MAOMBI: **37%**
2. UCHUNGUZI WANGU BINAFSI MTANDAONI AU KWENYE VITABU: **26%**
3. MAZUNGUMZO NA WAZAZI WANGU:**18%**
4. MAFUNDISHO KUTOKA KWA VIONGOZI WA DINI: **12%**
5. MAZUNGUMZO NA MARAFIKI: **8%**

India ilikuwa nchi pekee ambapo mwitikio kwenye swali hili ulijibiwa tofauti. Karibia nusu (46%) ya vijana wa India walisema kuwa mazungumzo na wazazi yangeweza kubadilisha mawazo yao na uzoefu binafsi ulishika nafasi ya chini (15%).

Vijana wasio na dini wanategemea zaidi uchunguzi wao binafsi, lakini hata hivyo, wanasema watabadilishwa zaidi na uzoefu binafsi. Wakristo ni wepesi zaidi kuliko vijana wa dini zingine kusema kuwa uzoefu binafsi utabadilisha mawazo yao. Kati ya dini zote, Waislamu wanaweka mkazo kidogo juu ya uzoefu binafsi na mkazo zaidi kwenye mafundisho kutoka kwa viongozi wao wa dini. (Kumbuka Waislamu ndio kundi kubwa lililopo kwenye kundi la "dini zingine" hapa chini).

## WANAWEZA ZAIDI KUBADILISHA MAWAZO YAO KUHUSU DINI



# *Hitimisho*

Ilisaidia kuwasikia vijana moja kwa moja kuwa ni sauti zipi za ushawishi na mwongozo wanazosikiliza katika ulimwengu ulio mkubwa na uliovurugika wanaoishi ndani yake. Haya ni baadhi ya mambo ya kutafakari juu ya mwitikio:

- **USHAWISHI WA FAMILIA UNA MAANA ZAIDI.**
  Utafiti huu unaonesha kuwa linapokuja suala la baadhi ya mambo muhimu ya maisha—vijana wanaziamini na hivyo kuzigeukia familia zao kwa mwongozo. Wazazi wana nafasi muhimu namna ambavyo mtoto anaenenda.

- **MAANDIKO NA KANISA YANA USHAWISHI MDOGO ZAIDI KULIKO VYANZO VINGINE.**
  Hili ni kweli zaidi linapohusisha mazungumzo kuhusu jinsia na ujinsia. Sauti za utamaduni huu zinasikika zaidi kupitia mitandao ya kijamii na kupitia rika na inaweka msimamo kwa vijana kwenye mada hizi muhimu. Ni kwa jinsi gani kanisa linaweza kujikita katika wajibu wake katika kuhusisha vijana kwenye maeneo haya muhimu?

- **UZOEFU BINAFSI UNA USHAWISHI ZAIDI KWENYE MAISHA YA VIJANA.**
  Vijana ambao tayari wanatembea na Kristo wanaendelea kuwa na kiu na uzoefu binafsi wa imani zao, na hata wale wanaosema Mungu hayupo, wapo tayari kubadilisha mawazo yao wakikutana naye. Tunawezaje kuwasaidia kuweka mazingira na fursa kwa uzoefu huo kutokea?



## BARUA KUTOKA KWA ROB HOSKINS

# *Je, tunasikiliza?*

Kwa mwanga wa utafiti huu, sasa tunafahamu vema ni nini kinachoshawishi vijana leo. Jukumu la kukikuza kizazi cha ki-Mungu katikati ya utamaduni usiokubali ukweli linaonekana kutowezekana, lakini Mungu wetu sio wa yasiyowezekana; Ni Mungu wa yasiyozuilika.

Japo inawezekana hatukupitia mambo yanayofanana katika kukua kwetu kama vijana wetu wanayopita leo, utafiti — kama ripoti hii —ni ufunuo. Kutokana nayo, tunaweza kuchimba mgodi wa uhalisia wa changamoto vijana wetu wanakabiliana nazo kila siku.

Kurasa hizi zimeweka wazi kuwa vijana wana shauku ya kupata ushauri wa hekima juu ya mada zilizochafuliwa kama jinsia na ujinsia. Viwango vya kushangaza vya mahangaiko binafsi na mawazo/majaribio ya kujiua kati ya vijana wetu ni kilio chao cha wazi kuwa wanahitaji msaada. Katika bahari hii vya machafuko, usikate tamaa kwani kuna habari njema! Vijana wanazitazama familia —za kibiolojia au kiroho—kama sehemu ya kwanza ya kugeukia wanapokuwa na maswali makubwa juu ya maisha yao.

Bahati mbaya, inaonekana kuwa badala ya kugeukia vyanzo halisi vya ukweli unaopatikana kwenye neno la Mungu, wachungaji, na Kanisa, vijana wetu wanaendea Google na YouTube kujifahamu wao ni nani na kusudi lao ni nini. Kuchanganyikiwa kwao sio kugeni. Kiuhalisia, nafikiri vijana leo karibia wanafanana na Tomaso mwenye shaka kwenye Yohana 14:5-6, alipouliza swali kubwa la maisha, “Tutaijuaje njia?”

Kadri vijana wetu wanavyojaribu kuuchunguza ulimwengu ambapo tamaduni zinapotosha na kushawishi, ni wajibu wetu kuwapa mwongozo kupata ukweli uliodumu vizazi vingi. Lazima tuwaelekeze kwa Yesu, anayekubali wasiwasi, kuvurugikiwa, na maswali yanaonekana kuwa sawa na yale ya wakati wa Tomaso. Kizazi kijacho kinataka kujua kuwa majibu yake hayapo hewani, lakini kuwa pamoja na kwamba ni makubwa, yanayochanganya, na yenye kutatiza ulimwengu iwezekanavyo, wanaweza mara zote kupata mwelekeo kutokana na usemi wake: “Mimi ndimi njia.”

*“Mimi ndimi njia.”*

# *Kuhusu OneHope*

Kwa ushirika na makanisa ya mahali, huduma na serikali ulimwenguni mwote, OneHope imewafikia zaidi ya watoto na vijana bilioni 1.6 kwa Neno la Mungu. Kupitia utafiti kwa kila nchi uonafanywa na OneHope, programu za maandiko huandaliwa kulingana na umri na utamaduni. Kuanzia 1987, OneHope imesaidia watoto wakutane na Hadithi ya Mungu, kushirikishana ujumbe wa tumaini kwa watoto na vijana wa kila nchi.
**onehope.net**

# *Njia ya utafiti*

Utafiti huu ulihusisha vijana 8,394 wa umri wa miaka 13-19 kwenye nchi 20. Katika kila nchi sampuli ya takribani vijana 400 waliotoa nguvu ya takwimu kuaminika kwa 95% kuwa matokeo ya 5% ya idadi ya vijana waliohojiwa kwenye umri wa 13 hadi 19, na kushabihiana na majaribio ya takwimu. Kwa maeneo mengi ya nchi na dunia nzima, kiwango cha kuaminika kilikuwa hata juu na kiwango cha chini kwa kukosea.

Kwenye nchi tano (China, Misri, India, Japan, and Vietnam), matengo ya sampuli yalifanywa ili kuhakikisha kuwa walau 10% ya waliohojiwa walikuwa Wakristo ili kupata ukubwa wa sampuli ambao unaendana na uchambuzi na ulinganifu wa kidini. Kwenye nchi kadhaa zingine, kiwango cha chini cha 10% ya ukubwa wa sampuli kwa Wakristo au Waislamu kilifikiwa au kukisiwa pasipo kutumia matengo ya sampuli. Matengo ya sampuli yalitumika Kenya kuhakikisha kuwa walau 40% ya waliohojiwa walikuwa wanawake.

Dodoso ziligawanywa kupitia Utafiti wa
Mwegemeo wa Maoni. Kwa kuthibiti ubora, wahojiwa walitolewa iwapo walijibu vibaya maswali rahisi ya kujaribu usikivu wao. Dodoso ilikuwa na maswali msingi 70, na maswali nyongeza yaliyolengwa kwa kila nchi kuchunguza kila mada husika.

# *Ukusanyaji wa Takwimu*

Takwimu za utafiti huu zilikusanywa kutoka Februari 24 hadi Machi 27, 2020. Tunaamini utafiti huu kwa usahihi unadhihirisha imani na tabia za vijana kabla ya kukumbwa na msambao wa athari za kujifungia kutokana na amri za karantini ambazo zingeathiri takwimu kutokana na muda uliotumika mtandaoni na afya ya akili kuashiria msongo, fadhaa, na mengine yaliyochunguzwa kwenye utafiti huu. Katika kila nchi isipokuwa tu China, ukusanyaji wa takwimu ulimalizika kabla ya kusitishwa kwa shughuli za kawaida kutokana na janga la Korona. China ilikuwa na upekee kwa kuwa kitovu cha janga hili na mwanzo kabisa wa hatua za kusitisha shughuli za kawaida.

| NCHI | UKUBWA WA SAMPULI | TAREHE ZA UKUSANYAJI WA TAKWIMU |
|---|---|---|
| Argentina | 420 vijana | Februari 27 - Machi 2, 2020 |
| Brazili | 420 vijana | Februari 27 - Machi 11, 2020 |
| China | 420 vijana | Februari 27 - Machi 6, 2020 |
| Colombia | 413 vijana | Februari 27 - Machi 2, 2020 |
| Misri | 420 vijana | Februari 27 - Machi 9, 2020 |
| India | 412 vijana | Februari 28 - Machi 17, 2020 |
| Indonesia | 420 vijana | Februari 27 - Machi 7, 2020 |
| Japani | 425 vijana | Februari 27 - Machi 23, 2020 |
| Kenya | 435 vijana | Februari 25 - Machi 27, 2020 |
| Mexico | 420 vijana | Februari 27 - Machi 2, 2020 |
| Uholinzi | 419 vijana | Februari 27 - Machi 8, 2020 |
| Nigeria | 420 vijana | Februari 24 - Machi 20, 2020 |
| Ureno | 419 vijana | Machi 7 - Machi 18, 2020 |
| Romania | 420 vijana | Februari 28 - Machi 13, 2020 |
| Urusi | 418 vijana | Februari 27 - Machi 2, 2020 |
| Afrika Kusini | 420 vijana | Februari 24 - Machi 7, 2020 |
| Hispania | 420 vijana | Machi 7 - Machi 13, 2020 |
| Uingereza | 420 vijana | Februari 24 - Machi 3, 2020 |
| Marekani | 410 vijana | Februari 24 - Februari 29, 2020 |
| Vietnam | 423 vijana | Machi 13 - Machi 26, 2020 |

# *UFAFANUZI*

### WAKRISTO IMARA

Vijana waliojitambulisha binafsi kama Wakristo, lakini sio Mashahidi wa Yehova au Mormon na waliotimiza vigezo vifuatavyo:

- Wanaamini kuwa Mungu yupo na wanaweza kuwa na mahusiano binafsi naye.
- Wanaamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu.
- Wanaamini kuwa msamaha wa dhambi unapatikana tu kupitia imani katika Yesu Kristo.
- Wanaamini kuwa Biblia ni Neno la Mungu.
- Wanajisomea Maandiko wenyewe kila siku au kwa wiki.
- Wanaomba kila siku au kila wiki.

Fahamu kuwa vijana Wakristo Imara wanaweza kuwa Wakatoliki, Wasabato, Orthodox au dhehebu lingine lolote la Kikristo.

### WAKRISTO WA KAWAIDA

Vijana waliojitambulisha binafsi kama Wakristo, lakini sio Mashahidi wa Yehova au Mormon na ambao hawatimiza vigezo vya imani thabiti au vipengele vilivyowekwa kwa Wakristo Imara.

### DINI ZINGINE

Vijana waliojitambulisha wenyewe kama Wabudha, Wahindu, Wayahudi, Waislamu, au dini zingine.

### WASIO NA DINI

Vijana waliojitambulisha wenyewe kama Wasioamini Mungu yupo, Wanaoamini Mungu hawezi kutambulika, au wasiofungamana na lolote kati ya hayo.

## MASWALI?

Maswali juu ya utafiti huu? Wasiliana na research@onehope.net

Utamaduni wa Vijana Duniani, Taarifa ya Dunia
Copyright © 2021 by OneHope, Inc.
600 SW Third Street Pompano, FL 33060
onehope.net
www.globalyouthculture.net

Nukuu ya Maandiko kutoka Biblia ya Habari Njema, 1995.
Copyright © 1995 by Bible Society of Kenya and Bible Society of Tanzania.
Haki zote zimehifadhiwa.
Biblia ya Habari Njema: 1995



# UTAMADUNI
## WA VIJANADUNIANI

OneHope
God's Word. Every Child.

OneHope, Inc. | 600 SW 3rd St. Pompano Beach, FL 33060 | 1-800-448-2425 | onehope.net